Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

**SWAHILI** **0262/02**

Paper 2 Listening **For examination from 2021**

SPECIMEN TRANSCRIPT **Approximately 35–45 minutes**

This document has **8** pages. Blank pages are indicated.

© UCLES 2018



https://xtremepape.rs/

Cambridge Assessment International Education
Cambridge IGCSE Specimen Examination in Swahili
Paper 2 Listening for examination from 2021
Turn over now

*(Pause 5 seconds.)*

**F:** **Zoezi 1**

**F:** Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

**F:** Swali 1

**M:** * Habari gani Roza? Hebu tuambie, wewe unaishi wapi?

**F:** Nzuri tu. Ninaishi Mombasa. Ni mojawapo ya miji mikubwa ya Kenya.

**M:** Je umeishi Mombasa kwa muda mrefu?

**F:** Ndiyo, maisha yangu yote. Wazazi wangu ni madaktari na nimezaliwa kwenye hospitali ambamo walikuwa wakifanya kazi. Walihamia Lamu miaka kumi iliyopita lakini mimi na dada yangu tumebaki hapa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 2

**M:** * Jana mama aliniuliza kuhusu mipango yangu kwa mwaka ujao, anataka nitume maombi kwenye vyuo vikuu nje ya nchi.

**F:** Bahati iliyoje! Wazazi wangu wanataka nibaki hapa Nairobi.

**M:** Nina hamu ya kusafiri nje ya nchi ingawa inanisikitisha kuiwacha familia yangu na rafiki zangu. Masomo ninayoyataka yanafundishwa Botswana tu.

**F:** Utakuja kututembelea na utapata rafiki wapya!

**M:** Bila shaka. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 3

**M:** * Tunaadhimisha uhuru wa nchi yetu kwa kutoa huduma za benki za simu bure. Kwa siku moja tu, wateja wataweza kufanya malipo na kupokea pesa kwa kutumia simu za mkono bila ya kutozwa pesa. Malipo yatakayofanywa na kupokelewa yanaweza kuwa ya kibinafsi na pia ya kibiashara. Tafadhali ufahamu kwamba kutuma ujumbe na kupiga simu kutatozwa kama kawaida. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

© UCLES 2018


https://xtremepape.rs/

**F:** Swali 4

**F:** * Je, umewahi kufikiria kuhusu kupanda mlima wa Kilimanjaro? Mlima ambao umesimama kipekee na wenye urefu wa mita 5895. Ni mlima mrefu zaidi kuliko yote barani Afrika! Lakini licha ya urefu wake, kuupanda si vigumu kwani kunahitaji uzima wa afya wa kawaida tu. Pata nafasi hii ya kujiunga nasi kwenye kuuchunguza na kuuelewa mlima huu wenye kilele chenye theluji na uliosimama juu ya mawingu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 5

**M:** * Habari za leo? Mimi ninaitwa James. Sipendi kusafiri na mabasi ya mjini kwani haya huwa na wasafiri wengi mno wakati wote. Pia kupata kiti cha kukalia huwa vigumu sana. Halafu mara nyingi foleni za magari huwa ndefu. Ningependelea sana kusafiri kwa miguu maana ningeweza kujenga afya yangu na ningeweza kufurahia mandhari ya mji. Lakini ninaishi mbali na kazini. Mwanzoni nilifikiri ninunue pikipiki lakini nilibadilisha mawazo kwa sababu ya kuogopa. Nimelazimika kusafiri kwa mabasi ya mjini. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 6

**F:** * Mambo! Jina langu ni Agnes. Wiki iliyopita niliona kitabu kinachoitwa ‘Kuhitimisha miaka 20 mjini Dar es Salaam’. Kinaonyesha picha za maisha ya vijana wakiendelea na shughuli zao za kila siku. Kilipigwa chapa zamani kidogo kwa hivyo sikushangaa kuona picha za mjomba wangu na shangazi yangu. Nilipigwa na butwaa kuona watu wa Dar zamani walifanya mambo tuyafanyayo sisi sasa hivi kama vile kusikiliza muziki na kucheza mpira. Nilitegemea kuona tofauti nyingi kati ya wakati wao na wakati wetu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 7

**M:** * Bi Kidude alipozaliwa aliitwa Fatuma Binti Baraka, lakini hakupendelea kutumia jina hilo katika kazi zake za kisanaa. Alikuwa mwimbaji maarufu wa muziki wa Taarab. Ingawa watu wengi wanamsifu Bi Kidude kwa uwezo wake mkubwa sana wa kuimba kwa kuchanganya lugha, mimi ninaupenda utu na ukarimu wake. Nyimbo ya ‘Mhogo wa Jang’ombe’ inaonyesha hasa uzuri wake. Katika nyimbo hii anawaasi vijana wawaheshimu wazee. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

**F:** Swali 8

**F:** * Zanzibar imekuwa ikishinda timu za Afrika ya Mashariki katika mashindano ya kombe la soka ya ufukweni. Na hivi jana ilinyakua kombe lenyewe kwa kuishinda timu ya Malawi. Jambo hili halijanishangaza hasa kwa vile kila siku wachezaji wa Zanzibar huimarisha ujuzi wao zaidi kwa kufanya mazoezi kwenye michanga ya ufukwe. Soka ya ufukweni ni maarufu sana kisiwani huko na kwa kawaida umati wa watu hukusanyika kuwatazama na kufurahia. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

**F:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

*(Pause 30 seconds.)*

**F: Zoezi 2**

**F:** Utamsikia msichana anazungumza kuhusu *Maonyesho ya Wiki ya Mitindo ya Kiswahili*.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

**F:** * *Wiki ya Mitindo ya Kiswahili* ni jukwaa muhimu kwa kuonyesha ubunifu wa mitindo barani Afrika. Mwaka huu jukwaa hili limeadhimisha miaka kumi tangu kuundwa. Sherehe kubwa iliandaliwa katika Jumba la Makumbusho ya Taifa jijini Dar es Salaam. Jumba la Makumbusho ambalo lina nafasi kubwa lilichaguliwa kwa sababu lipo katikati ya mji. Kazi za wanamitindo 30 ambao ni wenyeji na wengine 13 ambao ni wa kimataifa zilionyeshwa.

**F:** Nilipata nafasi ya kuzungumza na mwanzilishi wa maonyesho, Bwana Mustafa Hassanali ambaye pia ni mwanamitindo. Alinifahamisha kwamba yeye alikuwa akihudhuria sherehe tofauti za mitindo duniani kote. Alisema kwamba, ingawa kulikuwa na wanamitindo wenye vipaji vikubwa, lakini wote walifanya kazi peke yao. Lengo lake lilikuwa ni kujenga ushirikiano kati yao. Siku moja, akiwa likizoni nchini Msumbiji, lilimjia wazo la kuanzisha tamasha la mitindo mjini Dar es Salaam. Alisema, ‘kutokana na uzoefu nilioupata kwenye maonyesho tofauti ambayo nimehudhuria, niliwaza kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kuunda jukwaa ambalo tungeweza kulitumia kujivunia ubunifu wetu wenyewe’. Hivyo alianza kazi ya kuigeuza ndoto hiyo kuwa halisi.

**F:** Kikwazo kikubwa kilikuwa ni kukosa fedha. Alizungumza na wafanya biashara tofauti, akijaribu kutafuta watakaokubali kutoa ufadhili na alifanikiwa. Pale mwanzoni alisikitika kwamba watu wengi hawakuhudhuria maonyesho hayo kwani hawakuwa na uzoefu wa majukwaa ya mitindo. Lakini, kutokana na juhudi na bidii yake, hivi leo maonyesho hayo yanajulikana kimataifa. Mimi ningefikiri labda Mustafa angejigamba kwa mafanikio haya, lakini nimeona hajivuni kabisa. Jambo hili limenivutia sana.

**F:** Mustafa anaongelea umuhimu wa maonyesho haya katika kutoa fursa kwa vijana kuonyesha vipaji vyao. Pia, ili kuwapa nafasi, Mustafa mwenyewe haonyeshi miundo yake wakati wa maonyesho ya Wiki ya Mitindo ya Kiswahili. Lengo lake ni kujenga chapa madhubuti ambayo ni ya Kiafrika na itakayoimarishwa zaidi kwa kupitia jukwaa hili la mitindo. **

*(Pause 30 seconds.)*

**F:** Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

**F:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

*(Pause 30 seconds.)*



https://xtremepape.rs/

**F:** **Zoezi 3**

**F:** Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu maisha ya mjini na kijijini.

Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha A–G. Kwa kila msemaji, andika herufi (A–G) katika mstari wa jibu.

Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.

Utasikia rekodi mara mbili.

**F:** * Msimulizi 1

**M:** Nimeishi maisha yangu yote shambani. Nilikuwa mkulima wakati wote huo. Nimemwoa mwanamke wa kijiji chetu, nasi tumejenga unyumba hapa. Sasa nimestaafu, na ingawa sifanyi kazi ya ukulima, bado naendelea kuishi hapa. Najihisi sasa nimezeeka sana: hivyo sina azma yoyote ya kutenda mambo yasiyo ya kawaida yangu. Tena, maisha ya mjini hayatanifaa. Sitayapenda, ingawa baadhi ya marafiki zangu wanasema hayo ni maisha ya starehe.

**F:** Msimulizi 2

**F:** Hapa hakuna jambo la kufanya la starehe na kujiburudisha nyakati za magharibi na wikiendi. Ndio, kwenda shuleni ni sawa tu – kwani nina marafiki zangu hapo na tunajichangamsha kwa michezo na kupiga soga – lakini nje ya shule … ah, bwana, hakuna kitu! Labda ni sawa ikiwa wewe unapenda kutembea kwa miguu kwa muda mrefu. Lakini mimi sipendi. Mie napenda kwenda mahala kama mikahawani, sinema na madukani – yote unayoyapata mjini tu. Lakini itanibidi ningoje mpaka nimalize mitihani yangu kabla ya kwenda mjini. Nataka kwenda Chuo Kikuu mjini – hiyo ndio azma yangu. Na ikiwezekana sitarudi tena kijijini!

**F:** Msimulizi 3

**M:** Mimi nataka kulihama jiji hili – makelele, vumbi na mvuke wa petroli kutoka kwenye magari na mabasi yote hayo hunikasirisha sana. Ninapokwenda kuwazuru marafiki zangu wanaoishi mashambani, ninawaonea wivu ulioje! Wanaishi katika mazingira yenye hewa safi, tena hutembea huko kwa raha na starehe. Hata nafikiri hawapati mafua na magonjwa kila mara kama tupatavyo sisi tunaoishi mjini! Kwani tunapokezana magonjwa kwa vile watu wengi huwa tumejibana pamoja kwenye mabasi, matreni na maofisi. Ni rahisi kuambukizana magonjwa kwenye hali hiyo. Natumai siku moja nitaweza kutimiza ndoto yangu, lakini sifikiri. Haiyumkiniki.

**F:** Msimulizi 4

**F:** Ninapenda kuishi kijijini. Kijiji hiki ni kidogo sana. Mji mkubwa wa karibu nasi upo kiasi cha kilometa thelathini kutoka hapa. Na jiji lenyewe lipo mbali zaidi! Usifikiri ninachukia maisha ya jijini! La hasha! Nilipapenda tulipoishi jijini. Ninapenda kwa dhati mambo ya kihistoria! Na nilipoishi jijini nilipenda kuzuru makumbusho na maonyesho yote ya kihistoria. Lakini ikanibidi nihame huko, nihamie kwenye kijiji kidogo hiki! Hii ni kwa sababu nimebahatika kupata kazi niliyoitamani kwa muda mrefu! Kazi ya kuwa Mkurugenzi wa magofu yaliyopo kijijini humu. Wanafunzi wengi huja kwenye magofu na walimu wao. Kazi hii inanifurahisha sana na sijali hata kidogo kutoishi mjini.



https://xtremepape.rs/

**F:** Msimulizi 5

**M:** Hivi sasa nimestaafu kutoka kwenye kazi yangu ya kuwa Mkurugenzi wa Benki Kuu ya Taifa. Muda wote nilipokuwa mfanyakazi, imenibidi kuishi jijini kwa sababu ya kazi yangu. Na mke wangu pia alikuwa akifanya kazi benki. Lakini sasa – baada ya muda wote huu – tumepata bahati ya kuhamia shambani. Tuliipenda kazi yetu jijini lakini sasa tumefurahi kweli kuja kuishi shambani, mbali na ghasia na fujo za jijini!

**F:** Msimulizi 6

**F:** Tumehamia huku jijini – mume wangu, mimi, na watoto wetu – sasa inapata kufika kiasi cha miaka kumi. Tulifikiri na kuamua kwamba watoto wetu watafaidika na maisha zaidi hapa jijini – kwa vile kuna vitendo na shughuli nyingi za kuwakuza na kuwachachamua. Wanaweza kwenda kuogelea, kujiunga na vijana wenzao kucheza mpira na michezo mengine – O! kuna mengi ya kufanya hapa jijini. Tena ni rahisi sana kupata usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Mimi sijuti hata kidogo kuhama shamba na kuja kuhamia jijini! **

*(Pause 5 seconds.)*

**F:** Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

**F:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

*(Pause 30 seconds.)*

**F:** **Zoezi 4**

**F:** Utasikia mazungumzo kati ya Agnes na John.

Sikiliza mazungumzo hayo na soma maswali.

Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.

Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.

Utasikia rekodi mara mbili.

**M:** * Habari za asubuhi, Agnes. Sijakuona kwa muda mrefu sasa. Ulisafiri?

**F:** Sijambo, John! Ndiyo, nilikwenda Tanzania, nikakaa huko wiki mbili. Nilikwenda kuzuru mbuga za Manyara na Ngorongoro. Nilistarehe sana, na nimejifunza mengi pia. Hasa kuhusu wanyama na shida wanazokumbana nazo.

**M:** Kweli, wanyama wanakabili shida nyingi siku hizi.

**F:** Ingawa kwa baadhi ya watu ni vigumu kwao kuamini kwamba wanyama wanakabiliwa na shida zo zote. Wanafikiri wanyama wangeweza kuendelea kuishi tu kama kawaida bila ya msaada wo wote kutoka kwetu sisi binadamu.

**M:** Hivi unafikiri changamoto gani ndiyo ngumu zaidi kwao?



https://xtremepape.rs/

**F:** Mojawapo ya changamoto wanayokumbana nayo kila siku ni ile ya kukamatwa, kuuliwa na kuliwa na wanyama wengine. Pia hali ya hewa inabadilika – joto linaongezeka duniani, vyakula vinakuwa havitoshi, na tena ukame wa muda mrefu unawawia vigumu kwa wanyama kupata maji. Lakini pia kuna changamoto zingine ambazo, kwa mawazo yangu, ni kubwa kuliko zote. Hizo ni changamoto zitokazo kwa wanadamu, zinazotokana na vitendo vyetu – kama vile kuwinda. Kulikuwa na wakati katika historia yetu sisi wanadamu ambapo tulilazimika kuwinda ili kujipatia chakula. Lakini karne hizo zimepita.

**M:** Basi wewe hutaki watu wawinde wanyama pori kabisa?

**F:** Hapana, sikusema hivyo. Nikupe mfano. Tuseme mbwa mwitu mmoja anakuja kila usiku kula mbuzi au kuku wanaofugwa hapo na wanavijiji, basi ni sawa tu kumwinda. Hii ni kwa sababu anakuja kuharibu maisha ya wanavijiji. Lakini akiwa mnyama hawaingilii wanadamu hata kidogo – tuseme simba jike na wanawe akiwa mbali huko uwanjani – akijishughulisha na maisha yake tu – basi wanadamu hawana haki ya kumwinda na kumwua. Wanyama pia wana haki zao.

**M:** Kwa nini ni muhimu kwa wanyama kuwa na haki?

**F:** Kiini cha wazo hili ni kwamba wanadamu wawahifadhi wanyama wasipate maumivu au mateso ya bure. Kwa mfano, utamwona mtoto anamtupia mawe paka njiani. Sasa paka yule hakumfanyia mtoto yule lolote la kustahili apigwe. Mtoto anaona raha tu kumpiga! Basi ni muhimu yule mtoto ajue kwamba paka yule ana haki ya kutopigwa kwa mawe! Lakini kama paka akiiba samaki ambaye mtoto amemnunua kutoka kwa mvuvi, basi sawa, hapo mtoto ana haki ya kumfukuza paka, lakini hata hivyo, si kumpiga mawe!

**M:** Hayo ni maelezo mazuri! Tunahitaji kuwalinda wanyama wetu. Nimesikia kwamba kuna matatizo makubwa kuhusu viumbe kuwa hatarini kupungua. Kwa mfano, si idadi ya chui porini imepungua duniani kote?

**F:** Ndiyo! Ni kweli kabisa. Mwishoni mwa karne iliyopita wanasayansi walikadiria kwamba idadi ya chui wanaoishi maporini ilikuwa takribani 18 000. Lakini mwaka 2016 ilishuka kufikia 4000. Hivi sasa ni rasmi kwamba chui ni wanyama waliomo kwenye orodha ya wanyama walio hatarini kupotea kabisa duniani. Tena inategemewa kwamba katika miaka michache ijayo idadi yao itashuka zaidi na kuwa takribani 2000.

**M:** Hiyo ni tofauti kubwa mno. Nini sababu yake?

**F:** Sababu kuu ni kuharibiwa kwa makazi yao. Chui wanahitaji makazi tofauti kuishi: misitu, mbuga na sehemu za maji maji. Kama wanyama wengine, chui wanahitaji malazi, chakula na maji kwenye makazi yao. Miradi mikubwa ya ujenzi, ikiwa ni pamoja na hoteli huongeza changamoto kwenye makazi haya. Kinachosikitisha ni kwamba wageni kutoka nje ya nchi huja huku wakitegemea kuwaona chui porini na hawatambui kwamba kuja kwao ni mojawapo ya sababu ya kupotea kwa makazi. Serikali hazijachukua hatua za haraka ili kukwamisha tatizo hili.

**M:** Je kuna jambo lolote linalofanywa ili kuwasaidia chui?

**F:** Ndiyo. Ninafarijika kusema kwamba mashirika ya kitaifa na kimataifa yamekuwa yakishirikiana ili kusaidia uundaji na ulinzi wa makazi ambayo yatawafaa chui. Kwa hakika idadi ya chui imeongezeka kidogo katika miezi 12 iliyopita. Inategemewa kwamba idadi yao itaongezeka pole pole hadi kufikia 6000 mnamo mwaka 2022.

**M:** Vizuri sana.

**F:** Haya, naona bora niende zangu sasa. Nataka kwenda kuwachukua watoto wangu kutoka shule.

**M:** Nisalimie watoto. Pia wafundishe haki za wanyama! **



https://xtremepape.rs/

*(Pause 30 seconds.)*

**F:** Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

**F:** Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

That is the end of the examination.

*Copyright Acknowledgements:*

Dialogue 7: © *Mwimbaji Bi Kidude aaga Dunia Zanzibar*; BBC News Swahili; 17 April 2013.
Dialogue 8: © *Zanzibar National team wins Copa Dar es Salaam Beach Soccer Cup*; Azania Post; 26 December 2017.
Exercise 2: Paul Owere; *Tanzania: Ten Years of Swahili Fashion Week*; All Africa; 8 December 2017. © Mwananchi Communications Limited, publishers of Mwananchi, The Citizen and Mwanaspoti.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

Cambridge Assessment International Education is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which itself is a department of the University of Cambridge.



https://xtremepape.rs/